WIZARA MASWALA YA HAKI YA MAREKANI

IDARA YA HAKI ZA WAHAMIAJI NA WAAJIRIWA

KITENGOCHA HAKI ZA KIRAIA

HABARI KUHUSU FOMU I-9 YA WAKIMBIZI NA WANAOHIFADHIWA

Kila mtu anayeanza kufanya kazi kama mfanyakazi wa Marekani anajaza Form I-9 (Fomu I-9). Hii ni fomu ya serikali ambayo waajiri hutumia kuthibitisha utambulisho wakona ruhusa ya kufanya kazi. Fomu hii ni ya kusaidiawanaohifadhiwa na wakimbizi. Kwa hivyo, jaza Fomu ya I-9 na katika mchakato huu utajua haki zako. Wakati wa mchakato huu, waajiri wanaokubagua kwa misingi ya hali yako ya uraia au utaifa wako,wanaweza kukiuka sehemu ya Sheria ya Uhamiaji na Uraia. Sheria hii ya kupinga ubaguzi inapatikana katika sheria ya 8 U.S.C. sura ya 1324b, na kanuni za sheria hii yiko katika 28 C.F.R. Part 44 (28 C.F.R. Sehemu ya 44).

Toa taarifa zinazokuhusu katika Sehemu ya 1 ya fomu ya I-9.

Weka majina yako na habari nyingine kukuhusu katika Sehemu ya 1. Unaweza kuuliza mtu mwingine akusaidie kujaza sehemu hii. Lazima uweke alama inayoonyesha hali ambayo inakupa ruhusa ya kufanya kazikatika kisanduku. Wakimbizi na wanaohifadhiwa huchukuliwa kuwa “wageni wenye mamlaka ya kufanya kazi”. Kwa hivyo, weka alama katika kisanduku hiki. Kuna nafasi ya tarehe ya kumalizika muda karibu na kisanduku hiki. Kwa sababu haki yako ya kufanya kazi ni ya kudumu, andika “N/A” (ambayo ina maana “haiwezi tumika”) katika nafasi ya tarehe ya kumaliza muda. Unaweza kupata maelezo zaidi juu ya kujaza Sehemu ya 1 katika Form I-9 instructions (maagizo ya fomu I-9) au kwa kupiga simu katika Immigrant and Employee Rights Section (Idara ya Haki za Wafanyikazi na Wahamiaji)(IER) au U.S. Citizenship and Immigration Services (Huduma za Uhamiaji na Uraia wa Marekani) (USCIS).

Katika Sehemu ya 2 ya fomu ya I-9, ni lazima uonyeshe nyaraka za mwajiri wako ambazo zinathibitisha utambulisho wako na ruhusa ya kufanya kazi.

Fomu ya I-9 ina orodha tatu za nyaraka ambazo unaweza onyesha - List A (Orodha ya A) (nyaraka zinazoonyesha utambulisho wako na ruhusa ya kufanya kazi), List B (Orodha ya B) (nyaraka zinaonyesha utambulisho wako) na List C (Orodha ya C) (nyaraka zinaonyesha ruhusa ya kufanya kazi). Lazima uonyeshe mwajiri uchaguzi wako kama nimandiko ya Orodha ya Aau mwunganishowa Orodha ya B na C.

Katika Form I-9 instructions na regulations (maagizo na masharti ya fomu I-9) na kanuni za Fomu I-9, nyaraka nyingine zinazojulikana kama risiti zinakubalika kwa muda tofauti kwa Fomu ya I-9. Unaweza kupata maelezo zaidi juu ya mahitaji ya Fomu ya I-9 kwa kuwasiliana na IER au USCIS katika sheria ya 8 USC sura ya 1324a(b)(1)(A).

Una haki ya kuchagua nyaraka halali unayotaka kuonyesha. Mwajiri wako haruhusiwi kukulazimisha kuonyesha nyaraka maalum kulingana na hali yako kama muhifadhiwa au mukimbizi, au kwa kuzingatia asili yako ya kitaifa, na mwajiri akihitaji hati maalum inaweza kuwa ni ubaguzi kwa kuwa nu ukiukaji wa sheria. Hii sehemu ya sheria hupatikana katika sheria ya 8 USC sura ya 1324b(a)(6).

Kwa mfano, ingawa wewe una Hati ya Ajira, I-766 (EAD), unaweza kuamua kuonyesha nyaraka nyingine kama kitambulisho cha hali (hatiya Orodha B) na kadi isiyozuiliwa ya Usalama wa Jamii (hati ya Orodha ya C). Pata maelezo zaidi juu ya haki yako ya kuchagua nyaraka kwa kuwasiliana na IER.

Unaweza kuwa na aina ya nyaraka kadhaa halali za Fomu I-9.

Unaweza kuonyesha I-94 kwa Fomu I-9. Unaweza kupata kadi yako ya I-94 au unaweza kuchapisha I-94 yako kwenye tovuti ya Customs and Border Protection (Ulinzi wa Mpaka na Forodha).

Ikiwa wewe ni mwakimbizi, your I-94 is a receipt (I-94 yako ni risiti) ya hati ya Orodha A ambayo ni halali kwa siku 90 kutoka siku yako ya kwanza ya kazi. Baada ya siku 90, lazima uonyeshe EAD au hati ya Orodha ya B na Kadiisiyozuiliwa ya Usalama wa Jamii. Pata maelezo zaidi kuhusu kutumia nyaraka ya mkimbizi I-94 kwa kuwasiliana na IER katika sheria ya 8 C.F.R. 274a.2(b)(1)(vi)(C).

Ikiwa wewe ni mkimbizi, unaweza tumia I-94 kama a permanent List C document (hati ya kudumu ya Orodha C) ambayo haimalizi muda wake.

Wahifadhiwa na wakimbizi wanastahiki EAD. Ikiwa EAD yako imekwisha muda lakini uliomba iongezwe muda, unaweza kuendelea kufanya kazi na EAD yako iliyopo. Siku 180 baada ya kumalizika kwa EAD yako, unaweza kuionyesha ikiwa imeambatana na taarifa ya risiti ya I-797C inayoonyesha kuwa serikali imepokea maombi yako ya kuifanya upya. Kwa habari zaidi, piga simu kwa IER.

Unaweza pia kuonyesha risiti za lost, damaged or stolen (hati zilizopotea, zilizoharibika au zilizoibiwa) kwa sababu ya kazi ambazo hudumu zaidi ya siku mbili.

Mara baada ya kuonyesha nyaraka zako za kujaza Fomu ya I-9, si wakati mwingi mwajiri ataruhusiwa kukuuliza nyaraka tena. Sheria za wakati mwajiri lazima aomba hati tena zimejadiliwa katika Handbook for Employers (Kitabu cha Maagizo kwa Waajiri) katika ka sheria 8 C.F.R. 274a.2(b)(1)(vii).

Ikiwa umeonyesha EAD yako kwa sababu ya Sehemu ya 2, mwajiri wako atakuomba hati nyingine wakati muda wa EAD yako utakapomalizika ili ujazeSehemu ya 3 ya fomu ya I-9.Unaweza kuchagua kuonyesha hati halali ya Orodha A au C, kama vile kadi ya Usalama wa Jamii isiyozuiliwa. Waweza chagua kuonyesha EAD mpya lakini si lazima ufanye hivyo.

Ikiwa umeonyesha kadi ya Usalama wa Kijamii kwa sababu ya Sehemu ya 2 kama ushahidi wa ruhusa yako ya kufanya kazi na kukiwa kuliandikwa “N/A” kwa eneo la muda wa kumalizika karibu na “alien authorized to work” (mgeni aliyeidhinishwa kufanya kazi) katika Sehemu ya 1, mwajiri wako hana haja ya kuona nyaraka zako tena. Waajiri wanaowaomba nyaraka kulingana na hali yako ya kuwa muhifadhiwa au mukimbizi au kulingana na asili yako ya kitaifa wakati haihitajiki anaweza kuwa anakiuka sheria. Unaweza kupata habari zaidi juu ya sehemu hii ya sheria kwa kuwasiliana na IER kuhusu sheria katika U.S.C 8 sura ya 1324b(a)(1) au (a)(6).

Huna haja ya kuwa na nambari ya Usalama wa Jamii ili kuanza kufanya kazi.

Ikiwa umepata kazi na bado hujapata nambari yako ya Usalama wa Jamii (SSN), Social Security Administration (Idara ya Usalama wa Jamii) inawashauri waajiri kuwa wafanyakazi wanaruhusiwa kufanya kazi huku wakisubiri SSN.

Ni lazima Mwajiri wako akulipe kwa kazi yako hata kama bado unasubiri SSN. Sheria ya Viwango vya Kazi ya Haki, inayopatikana katika U.S.C 29 sura ya 201, inakupa haki ya kulipwa kwa kazi zote unazofanya.

Ikiwa huna SSN yako wakati unapoanza kazi,katika Sehemu ya 1, acha kisanduku cha SSN kikiwa tupu. Hii ni kweli hata kama mwajiri wako anatumia E-Verify.

Idara ya Haki za Wahamiaji na Waajiriwa (IER)

1-800-255-7688

www.justice.gov/ier

Kwa kuwa lugha yaweza kuwa haijulikani,huduma za lugha zinapatikana.

TTY 1-800-237-2515

Kipeperushi hiki si hatuaya mwisho ya shirika, haina athari ya kisheria na inaweza kuondolewa au kurekebishwa kwa hiari ya Idara na kwa mujibu wa sheria zinazohusika. Kipeperushi hakionyeshi kisheria majukumu ya kutekelezwa kuliko yale yanayohitajika na masharti ya sheria husika, kanuni, au mfano wa mahakama ya kisheria.